



TANGAZO LA MAENEO YA KUPANGA KWA AJILI YA KUTOLEA HUDUMA KWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) kinapenda kuutangazia umma kuwa kimetenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

Na.	ENEO	KAMPASI/MAHALI	HUDUMA INAYOTAKIWA
1.	Chumba Namba 1, Hall IV - Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Saluni ya Kiume
2.	Chumba Namba 2, Mabibo Shopping Complex	Hosteli za Mabibo	Steshenari na kuchapisha nyaraka, kadi za mwaliko n.k.
3.	Kampasi ya Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano (Kuanzia tarehe 31 Januari 2023)	Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano	Mgahawa mdogo wa chakula

Kwa tangazo hili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawaalika wale wote wenye nia na wanaopenda kutoa huduma hizo kama zilivyoainishwa katika jedwali hapo juu kuomba kutoa huduma. Waombaji wafike Kurugenzi ya Mipango, Mendeleo na Uwekezaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Ofisi Namba 303 Jengo la Utawala (Cranford Pratt Building) kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi. Waombaji watalipa Shilingi elfu kumi tu (**TZS 10,000/=**) kupitia 'Namba ya Kumbukumbu' ambayo inapatikana Ofisi Namba 225 kwa Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Mwisho wa kuchukua fomu na kurudisha ni siku kumi na nne (14) kutoka siku ya kwanza ya tangazo hili.

Tarehe **5 Decemba 2022** itakuwa ni siku ya kutembelea maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutolea huduma hizo ambapo saa 4:00 asubuhi tutakutana katika Kampasi ya Mikocheni, saa 6:00 mchana tutakutana katika Hosteli za Mabibo na kuanzia saa 8:00 mchana tutakutana katika Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani.

Baada ya mchakato wa kupata watoa huduma kukamilika, waombaji wote wataarifiwa juu ya matokeo hayo kwa njia ya barua.

Imetolewa na
NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – MIPANGO, FEDHA NA UTAWALA
28.11.2022